



KONGAMANO LA ISHIRINI NA NNE LA KISWAHILI **Bayreuth, tarehe 03 hadi tarehe 05 mwezi wa sita 2011**

Tarehe 27, mwezi wa
Januari, 2011

Wapendwa mabibi na mabwana!

Tuna furaha kubwa kuwaalika kwenye kongamano la ishirini na mbili litakayofanyika hapa Ujerumani katika Chuo Kikuu cha Bayreuth.

Kongamano letu la Kiswahili limeshaota mizizi hapa katika Chuo Kikuu cha Bayreuth. Kila mwaka linawakaribisha watalamu wa masomo mbalimbali wanaofanya uchunguzi kuhusu vipengele kadha vya Kiswahili (ama Viswahili) na tamaduni zao. Upana wa mada zinazohusu Kiswahili na zinazozungumziwa kwenye Kongamano, kuanzia isimu, masomo ya fasihi mpaka anthropolojia na historia ni msingi wa nguvu ya kongamano hili. Watalamu kutoka pembe mbalimbali za dunia na masomo tofauti wanapata kubadilishana mawazo. Pia tunawakaribisha washabiki na wasanii wa fani mbalimbali za Kiswahili. Zaidi ya kuwakaribisha wale ambao wamezoea kuja Bayreuth, pia tunafurahi kuwakaribisha watalamu na wanafunzi wapya kwetu.

Mada maalum

Mwaka huu, Kongamano la Kiswahili litakuwa na mada maalum, '**Kiswahili na Usasa**'. Mada hii inapendekeza kuchunguza na kujadili mikondo ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa ilizaliwa ama ilipata nguvu katika karne ya ishirini. Mwangalio huo unasisitiza vipengele vya mabadiliko yanayotokea katika nyanja mbalimbali, kama mfumo na matumizi ya lugha ya Kiswahili, katika mitindo na mada za fasihi, lakini vilevile katika mabadiliko ya jamii yenyewe na utamaduni wake. Kwa hivyo tunaalika michango kutoka sehemu mbalimbali za utafiti ili kuzua mjadala mpana.

'Kiswahili na Usasa' itakuwa ni mada maalum kwa kongamano lifuatalo itakayopewa nafasi maalum. Lakini, kupendekeza mada maalumu hakumaanishi kwamba hatutakubali mada nyingine. Ikiwa unapendelea kuzungumzia mada nyingine, pia usisite kujiandikisha.

Kujiandikisha

Tunaomba mada zenu katika lugha ya Kiswahili ama Kiingereza. Kila uwasilishaji wa mada pamoja na majadiliano unakadiriwa kuchukua muda wa dakika thelathini tu. Tafadhalini, mjiandisheni kwa njia ya baruapepe (swahili@uni-bayreuth.de) mpaka kufikia tarehe **30 Machi 2011**. Iwapo mtatoa makala yenu kwa Kiswahili, tafadhalini muandike pia muhtasari mfupi kwa Kiingereza. Tafadhalini, mjiandikishe pia hata ikiwa hamutatoa makala.

Pahala/wakati

Pahala pa Semina hii patakuwa Iwalewa-Haus, Münzgasse 9. Semina itaanza siku ya Ijumaa tarehe 03, mwezi wa sita, saa tatu asubuhi na itamalizika Jumapili tarehe 05. Kumalizika kwa kongamano kutategemea idadi ya mada tutakazozipokea.

Muda si mrefu unaweza kupata barua hii, ratiba na habari mpya kwenye ukurasa wa mtandao ufuatao:

http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq1/index.html

Malazi

Kwenye ukurasa wa mtandao mtapata habari za malazi. Iko orodha ya hoteli pia (maelezo hayo yanatokana na Idara ya Utalii ya mji wa Bayreuth). Tena wanafunzi wetu watawakaribisha wanafunzi kutoka vyuo vikuu vyingine wakae nyumbani mwao kwa muda wa kongamano. Wanafunzi wanaotaka kupata malazi kwa mtu binafsi, watuarifu mapema kwa njia ya baruapepe (tazama anwani yetu chini). Tena, wanafunzi (chini ya umri wa miaka 25) wanaweza kupata malazi katika “Bweni la Vijana” (tazama <http://www.jugendherberge.de/jh/bayern/bayreuth/>).

Tunapenda kuwaarifu kwamba suala la malazi na chakula mtajitegemea.

Barua ya pili ya mwaliko itakayoambatanishwa na mpangilio wa makala na utaratibu mzima wa semina itatumwa mwisho wa mwezi wa nne (Aprili).

Ikiwa mna maswali, msisite kutuandikia. Kwa mawasiliano zaidi, tumieni anwani yetu ya email: **swahili@uni-bayreuth.de**.

Tukiwa na matumaini ya kuonana katika Kongamano hili la 24 la Kiswahili hapa Bayreuth twasema “Karibuni Sana.”

Prof. Gabriele Sommer, Dr. des. Clarissa Vierke

Prof. Said A. M. Khamis

Afrikanistik I
Universität Bayreuth,
95440 Bayreuth
Tel.: +49-921-553556
Fax.: +49-921-553627

Literaturen in afrikanischen Sprachen
Universität Bayreuth,
95440 Bayreuth
Tel.: +49-921-553598
Fax.: +49-921-553641